# Kuandika

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Pili



Taasisi ya Elimu Tanzania

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kuandika

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Pili



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

Cheti cha Ithibati

Na. 2

Jina la Chapisho: Kuandika Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Pili

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978 - 9976 - 61 - 702 - 3

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 19 Mwezi Januari Mwaka 20 18 kuwa kitabu cha Kiada kwa ajili ya Darasa la Pili katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2015.

Dkt. Edicome Cornel Shirima
Kaimu Kamishna wa Elimu.

## Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY

Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 1 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la kwanza 2018
Chapa ya Pili 2021

ISBN 978 - 9976 - 61 - 702 - 3

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam
Simu +255 735 041 170 / +255 735 041 168
Baruapepe director.tie@tie.go.tz
Tovuti www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kupiga chapa, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 2 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Utangulizi**......................................................iv
**Shukurani**.....................................................v

**Sura ya Kwanza**

Kuumba herufi.................................................. 1

**Sura ya Pili**

Kuunda maneno............................................... 12

**Sura ya Tatu**

Kupanga na kuandika sentensi katika
mtiririko sahihi..................................................21

**Sura ya Nne**

Matumizi ya alama za uandishi...........................29

**Sura ya Tano**

Kuandika habari fupi.........................................34

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 3 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kujua kuandika ni muhimu katika kujifunza. Ukijua kuandika, utajifunza mambo mbalimbali na kuyaandika. Ulipokuwa Darasa la Kwanza, ulijifunza kuandika herufi mchangani. Uliweza kunakili, kuigizia na kufuatisha picha na herufi. Ulianza kuumba herufi kwa kuchora michoro ya herufi. Uliweza pia kuandika maneno na sentensi.

Kitabu hiki kitakuwezesha kujua kuandika vizuri. Utajifunza kuumba herufi, kuunda maneno na kuandika sentensi kwa mwandiko wa kuunga. Utaweza pia kuandika habari fupi zenye maana.

Soma kwa makini habari zilizomo kitabuni na uzielewe. Soma maswali na mazoezi uliyopewa. Jibu maswali kisha fanya mazoezi yote. Unaweza kupata msaada kwa watu mbalimbali. Unaweza kuwauliza wenzako, wazazi au walimu wako.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 4 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi na maandalizi ya kitabu hiki.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki wakiwemo wachapaji, wasanifu, wahariri, wachoraji na wapiga chapa. Pia, inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa maudhui na uhariri wa kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kutayarisha na kuchapa kitabu hiki.

Mwisho, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa ukaribu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.



**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

FOR ONLINE USE ONLY

Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 6 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Kuumba herufi

Katika sura hii utajifunza kuumba herufi. Vilevile, utajifunza kuandika mwandiko wa kuunga.

### Zoezi la Marudio

1. Soma kisha nakili silabi hizi.

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ra | ya | no | zi | di | lu | si | mi | ze | ki | chu |
| da | to | bi | fu | bo | ga | fa | he | jo | ka | lo |
| ne | pi | re | su | te | vi | vo | we | wi | yu | mo |
| ge | ho | pe | ju | che | nye | sha | sho | kwi | kwe | mwe |
| mwa | ndo | ndi | nzu | nzi | tha | | | | | |

2. Andika maneno kumi kutokana na silabi ulizonakili.

**Mfano**

ndizi, refu, boga

3. Soma kisha nakili sentensi hizi.

Naomi anasoma darasa la pili.
Shule yetu ina madarasa tisa.
Mama ni mpishi shuleni.
Choo cha shule yetu kina matundu sita.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 1 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Michezo inajenga afya.
Tutumie vyandarua kujikinga na malaria.
Juma na Lulu wanachemsha chai.
Nunua kalamu mbili dukani kwa Omari.

4. Tunga sentensi nne sahihi kutokana na maneno yaliyomo kwenye jedwali.

**Mfano** Amina ni mwanafunzi.

| | | |
|---|---|---|
| Amina<br>Juma | ana<br>ni | daktari wa meno<br>mwanafunzi<br>mkimbiaji<br>kitabu cha michezo<br>machungwa matano |

## Somo la kwanza

### Kuandika herufi za mwanzo za majina ya matunda, wanyama na vifaa vya ndani

Katika somo hili utaandika herufi za mwanzo za majina ya matunda. Vilevile, utaandika herufi za mwanzo za majina ya wanyama na vifaa vya nyumbani.

FOR ONLINE USE ONLY




Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 2 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


Tazama picha zifuatazo kisha jibu maswali.

## Picha ya matunda



1. Andika majina ya matunda yaliyopo juu ya meza.
2. Chora picha za matunda yaliyopo mezani.
3. Andika herufi ya kwanza ya kila tunda.

## Picha ya wanyama



FOR ONLINE USE ONLY




Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 3 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Taja majina ya wanyama unaowaona katika picha hii.
2. Andika jina la mnyama mkubwa kuliko wote.
3. Andika herufi ya mwanzo ya kila mnyama unayemwona.

## Picha za vifaa vya nyumbani



1. Andika majina ya vitu unavyoviona.
2. Andika herufi za mwanzo za vitu unavyoviona.
3. Andika mistari miwili ya herufi **m** na **k.**

## Zoezi la kwanza

Andika kwa mwandiko wa chapa.

1. Herufi za mwanzo za majina ya vyakula unavyovipenda.

   ........................... ...........................

2. Herufi za mwanzo za majina ya rangi unazozijua

   ........................... ...........................

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 4 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Somo la pili

### Kuumba herufi za kuunga

Katika somo hili utajifunza kuandika herufi za kuunga. Herufi zinapoandikwa huungwa upande wa kushoto. Pia, zipo zinazoungwa kushoto na kulia. Herufi nyingine haziungwi.


### Herufi zinazoungwa upande wa kushoto tu.

Herufi zinazoungwa upande wa kushoto tu ni b, g, j, o, p na y.

Nakili herufi zifuatazo katika daftari lako.

b, g, j, o, p na y.

**Mfano**




FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 5 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la pili

Andika silabi **yo, go**, **bo, jo** na **po** kwa kuunga kushoto.

## Zoezi la tatu

Andika maneno haya kwa mwandiko wa kuunga **jojo, popo, yaya** na **boya.**

## Herufi zinazoungwa kulia na kushoto.

Herufi zinazoungwa kulia na kushoto ni

**a, ch, d, e, h, i, k, l, m, n, t, r, u, v, w**

Nakili herufi zifuatazo katika daftari lako.

**a, ch, d, e, h, i, k, l, m, n, t, r, u, v, w**

**Mfano**

a ch d e h i k l


m n t r u v w

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY


Nakili mchoro unaoungwa kulia na kushoto.

**Mfano**



Nakili michoro ya herufi zifuatazo inayounga kushoto kwenda kulia. **e, h, i, k, r, u**

**Mfano wa michoro**



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

rrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrrr

uuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuuu

## Zoezi la nne

Andika silabi zifuatazo kwa mwandiko wa kuunga.

**la, me, di, ka, ba, cha, pi, go, jo, sha, ndo, kwi, nyi, wa, thu, ha, ni, to, da, ma, mwa, nwe, dhu, ro, vi** na **ta**

## Zoezi la tano

Andika maneno haya kwa mwandiko wa kuunga **acha, mama, dada** na **chama**.

## Herufi ambazo haziungwi.

Herufi ambazo haziungwi ni **f, s** na **z**

Nakili herufi zifuatazo katika daftari lako.

f f f f f f f f f f

**s s s s s s s s s s**

**z z z z z z z z z z**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la sita

Andika silabi **fa, se,** na **zu.** Hakikisha kila silabi inajaa katika mstari wake.

## Somo la tatu

### Kuandika maneno kwa mwandiko wa kuunga

Katika somo hili utaandika maneno kwa mwandiko wa kuunga.

Nakili maneno yafuatayo kwa mwandiko wa kuunga.

tembo begi ondoa

kondoo papai kitanda

lala hema punda

Nakili michoro hii.

kkkkkkkkkkkkkkkkkkkkkk

memememememememememememememememe

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 9 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nenenenenenenenenenenenenenenenene

hahahahahahahahahahahahaha

papapapapapapapapapapapapapa

## Zoezi la saba

Nakili maneno yafuatayo kwa mwandiko wa kuunga.

| | | |
|---|---|---|
| Kigoma | Mtera | Kaskazini |
| Dawati | Kusini | Mbeya |
| Magharibi | Mnyororo | Themanini |
| Mashariki | Mnyama | Nzi |

## Zoezi la nane

Andika maneno yafuatayo kwa mwandiko wa kuunga.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ishirini | kausha | Rukwa | matunda |
| mwanafunzi | nyanya | ndogo | theluthi |
| mkono | zamani | kwaruza | barabara |

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 10 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la tisa

Andika majina yafuatayo kwa mwandiko wa kuunga.

Anusiata, Selemani, Jerome na Hadija.

## Zoezi la kumi

Andika sentensi zifuatazo kwa mwandiko wa kuunga.

**Mfano**

*kaka na dada wanasoma*

1. Baba na mama wanalima.
2. Mwalimu wetu anaandika.
3. Wanafunzi wanaimba.
4. Popo anaruka.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Kuunda maneno

Katika sura hii utajifunza kuunda silabi na maneno. Utatumia konsonanti na irabu.

### Somo la kwanza

### Kuunda silabi kwa kutumia konsonanti mbili na irabu moja

Silabi huundwa kwa kutumia konsonanti na irabu. Katika somo hili utaunda silabi. Utatumia konsonanti mbili na irabu moja.

Mfano konsonanti **gw sw vy rw ng'** na irabu ( ***e o i u a*** ).

**Mfano wa silabi**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **gw** | na | **i** | zinaunda | **gwi** |
| **gw** | na | **e** | zinaunda | **gwe** |
| **ng'** | na | **o** | zinaunda | **ng'o** |

#### Zoezi la kwanza

Unda silabi kwa kutumia konsonanti **sw, vy, rw, py, nj, pw, fy, ng'** na irabu (**u, e, i, o, a**).

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 12 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Somo la pili

### Kuunda silabi ambatani zenye konsonanti tatu na irabu moja

Katika somo hili utaunda silabi ambatani. Utatumia konsonanti tatu na irabu moja.

Mfano wa konsonanti **ngw** **ndw** **mbw** **njw** **chw** **nyw** **shw** na irabu ( **i** **e** **a** **o** **u** )

**Mfano wa silabi**

**ngw** na **i** zinaunda **ngwi**
**ndw** na **e** zinaunda **ndwe**
**nyw** na **o** zinaunda **nywo**

### Zoezi la pili

Unda silabi kwa kutumia konsonanti **ngw** **ndw** **mbw** **njw** **chw** **nyw** **shw** na irabu (**u, e, i, o, a**).

**Mfano**

**ndwi, ndwu, ndwa, ndwe, ndwo**

## Somo la tatu

### Kuunda maneno kwa kutumia konsonanti

**b** **m** **k** **d** **n**

Katika somo hili utaunda maneno kwa kutumia konsonanti **b** **m** **k** **d** **n** na irabu ( **a** **e** **i** **o** **u** ).

**Mfano**

Herufi **d u m a** zinaunda neno **duma.**

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 13 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la tatu

Unda maneno kwa kutumia konsonanti **k** na **n** na irabu ( **a e i o u** ).

## Somo la nne

### Kuunda maneno yatokanayo na konsonanti **l t p s f j**

Katika somo hili utaunda maneno yenye maana. Utatumia konsonanti **l t p s f j** na irabu (**o u a i e** ).

**Mfano**

Herufi **j i t u** zinaunda neno **jitu.**

## Zoezi la nne

Unda maneno kwa kutumia konsonanti **l t p s f j** na irabu ( **a e i o u** ).

## Somo la tano

### Kuunda maneno yatokanayo na konsonanti **g y z h r w v ch**

Katika somo hili utaunda maneno yenye maana. Utatumia konsonanti **g y z h r w v ch** na irabu (**o u a i e**).

**Mfano**

Herufi **g a r i** zinaunda neno **gari.**



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 14 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la tano

1. Andika maneno matano yatokanayo na konsonanti hizi **g y z h r w v ch** na irabu (**a e i o u**).
2. Andika majina matatu ya vitu vinavyopatikana shuleni. Herufi zake za mwanzo ziwe kati ya **g y z h r w v ch d m k** na irabu (**a e i o u**).
3. Andika majina matatu ya vitu vinavyopatikana nyumbani. Herufi zake za mwanzo ziwe kati ya **g y z h r w v ch** na irabu ( **a e i o u**).

## Somo la sita

### Kuandika majina ya kwanza ya wanafunzi katika darasa

Katika somo hili utajifunza kanuni ya kuandika majina ya watu.

Majina ya watu huanza kuandikwa kwa herufi kubwa

**Mfano**

Yakobo, Ali, Maria, Halima.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 15 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la sita

Andika majina ya wanafunzi kumi katika darasa lako.

## Zoezi la saba

Tazama picha hii. Chagua marafiki zako wawili kisha jibu maswali.

Kujitambulisha kwa majina.



Mimi ninaitwa........... Wewe unaitwa ..................

na huyu anaitwa .....................

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 16 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuimba wimbo

Imba wimbo huu

Jieleze x6

Najieleza maamaa

Mimi hapa ndiye Asha

Baba yangu ni Baraka

Mama yangu ni Amina

Najieleza maamaa

### Zoezi la nane

1. Andika majina matatu yaliyotajwa katika wimbo hapo juu.
2. Tenga silabi katika majina hayo.
3. Nakili na tenga silabi katika maneno haya milima, taulo, mikuki na kitana.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 17 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Somo la saba

### Kuandika majina ya vitu mbalimbali


Katika somo hili utaandika majina ya vitu mbalimbali. Utatumia mwandiko wa kuunga.

Majina ya vitu mbalimbali huandikwa kwa herufi ndogo.

**Mfano**

kiti, chupa, shati.

Tazama picha hizi. Andika majina ya vitu unavyoviona.



### Zoezi la tisa

Jibu maswali haya. Andika kwa mwandiko wa kuunga.

1. Andika majina ya vitu vitano vilivyoko darasani kwako.
2. Andika majina ya vitu vitano vilivyoko jikoni kwenu.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 18 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Somo la nane

## Kuunda maneno yenye silabi zaidi ya nne

Katika somo hili utauunda maneno yenye silabi zaidi ya nne. Utatumia chati ya sakaneno.

### Zoezi la kumi

Tumia chati hii kuunda maneno sita yenye maana.

**Mfano**

baiskeli, msimamizi.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ba | ra | ba | ra | ni | ka |
| i | ka | m | zu | i | a |
| s | i | me | li | pi | wa |
| ke | ma | zo | e | zi | na |
| li | shu | hu | di | e | ha |
| ka | ni | e | le | ze | mi |
| e | l | i | g | za | si |
| li | be | ra | tu | si | ku |
| mi | me | sha | ku | ja | ta |
| she | shu | shi | e | ni | mbu |
| ni | mi | li | ke | ni | li |
| mwa | na | mi | che | zo | sha |
| m | si | ma | mi | zi | ba |

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 19 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Somo la tisa

### Kutunga sentensi zenye maneno yanayozidi sita

Katika somo hili utajifunza kutunga sentensi. Utatumia jedwali la maneno. Urefu wa sentensi hizo ni maneno zaidi ya sita.

### Zoezi la kumi

Andika sentensi sita kutoka kwenye jedwali hili.

| | | |
|---|---|---|
| 1. Baba na mama<br>2. Juma na Halima<br>3. Wanafunzi wote | wanalima<br>wanatoka | mtaa wa karibu<br>karanga na mtama<br>mtoni kuteka maji<br>shamba la mahindi<br>kule shambani<br>karibu na shule |

**Mfano**

Baba na mama wanalima shamba la mahindi.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 20 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Kupanga na kuandika sentensi katika mtiririko sahihi

Katika sura hii utapanga sentensi katika mtiririko sahihi. Utatumia picha na sentensi zilizochanganywa. Vilevile, utaandika hadithi fupi unayoifahamu. Hadithi itaandikwa kwa mtiririko sahihi wa matukio.

## Somo la kwanza

### Kuunda sentensi zenye mtiririko sahihi kwa kutumia picha

Katika somo hili utauunda sentensi zenye mtiririko sahihi. Utatumia picha.

### Zoezi la kwanza

Panga picha hizi kwa kufuata mtiririko wa matukio.

1.



FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 21 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2.



3.



Andika sentensi tatu kutokana na picha ulizopanga.

1. .................................................................
2. .................................................................
3. .................................................................




Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 22 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la pili

Panga picha hizi kwa kufuata mtiririko wa matukio.


**1.**




**2.**



**3.**



**4.**



Andika sentensi kufuata mtiririko wa matukio katika picha.

1. ..........................................................................
2. ..........................................................................
3. ..........................................................................
4. ..........................................................................

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 23 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Somo la pili

### Kupanga sentensi zilizochanganywa

Katika somo hili utajifunza kupanga sentensi zilizochanganywa. Lengo likiwa kupata sentensi zenye mtiririko sahihi.

**Mfano**

| Sentensi zilizochanganywa | Sentensi zilizopangwa |
|---|---|
| 1. Ninakwenda shuleni | 1. Ninaamka asubuhi na mapema |
| 2. Ninakunywa uji | 2. Ninapiga mswaki na kuoga |
| 3. Ninaamka asubuhi na mapema | 3. Ninavaa sare ya shule |
| 4. Ninavaa sare ya shule | 4. Ninakunywa uji |
| 5. Ninapiga mswaki na kuoga | 5. Ninakwenda shuleni |

**Zoezi la tatu**

Soma sentensi hizi kisha jibu maswali.

| | |
|---|---|
| 1. | Nyumba inafanyiwa matengenezo. |
| 2. | Watu wanatoa vyombo ndani ya nyumba. |
| 3. | Moto unawaka ndani ya nyumba. |
| 4. | Majeruhi wanapelekwa hospitalini. |
| 5. | Watu wanapiga mayowe. |
| 6. | Masalia ya vitu vilivyoungua yanatolewa nje. |

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 24 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1. Panga sentensi ulizosoma katika mtiririko wenye kuleta maana.
2. Andika sentensi hizo kwa mwandiko wa kuunga.

## Zoezi la nne

Andika sentensi tano kueleza matukio uliyoyafanya tangu ulipoamka.

**Soma habari hii.**



Hii ni bendera ya Tanzania. Bendera ya Tanzania ina rangi nne. Rangi hizo ni kijani, nyeusi, manjano na buluu. Rangi ya kijani inawakilisha mimea. Rangi nyeusi inamwakilisha mwafrika. Rangi ya buluu inawakilisha mito, maziwa na bahari. Rangi ya manjano inawakilisha madini. Bendera yetu inapendeza.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 25 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la tano

Panga sentensi hizi katika mtiririko wenye kuleta maana.

1. Rangi hizo ni kijani, nyeusi, manjano na buluu.
2. Watu wa Tanzania wanawakilishwa na rangi nyeusi.
3. Rangi ya manjano inawakilisha madini.
4. Maziwa, mito na bahari huwakilishwa na rangi ya buluu
5. Bendera yetu inapendeza.
6. Bendera ya Tanzania ina rangi nne.

## Zoezi la sita

Jibu maswali haya.

1. Bendera ya Taifa ina rangi ngapi?
2. Je, Bendera ya Taifa hupandishwa saa ngapi?
3. Bendera ya Taifa inapopandishwa unatakiwa kufanya nini?
4. Je, Bendera ya Taifa hushushwa saa ngapi?

# Somo la tatu

## Kuandika hadithi fupi kwa mtiririko wa matukio

Katika somo hili utaandika hadithi fupi unayoifahamu. Hadithi ifuate mtiririko wa matukio. Vilevile utasoma hadithi na kujibu maswali.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 26 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma hadithi ifuatayo kisha jibu maswali.**

## Umuhimu wa Maji



Siku moja dada na kaka walisafiri. Walikwenda kijijini kumuona babu yao. Babu alikuwa akiishi karibu na mto. Siku ya safari, waliondoka asubuhi na mapema. Walitembea kwa miguu mpaka kijijini kwa babu. Walikaa huko kwa muda wa wiki moja.

Wakiwa kwa babu walifanya kazi ya kuchunga mbuzi. Baada ya wiki moja maji yalipungua mtoni. Dada akauliza, kwanini maji yamepungua? Kaka akajibu, ni kwa sababu ya jua kali. Kama mvua haitanyesha miti itakauka yote. Angalia miti miwili imeanza kunyauka. Ahaa! Kumbe miti inakauka ikikosa maji? Sasa nimeelewa, nashukuru kaka kwa maelezo yako.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 27 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la saba

Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika.

1. Taja watu waliomtembelea babu.
2. Eleza sababu za miti kukauka.
3. Kaka na dada walifanya kazi gani kwa babu?
4. Umejifunza nini kutokana na hadithi hii?

## Zoezi la nane

Jibu maswali hayo.

1. Andika hadithi fupi unayoifahamu.
2. Hadithi hiyo inatufundisha nini.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 28 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Matumizi ya alama za uandishi

Katika sura hii utaandika sentensi fupi, habari na hadithi fupi. Utatumia alama nne za uandishi.

Alama hizo ni mkato (,), nukta (.), alama ya mshangao (!), na alama ya kuuliza (?)

### Somo la kwanza

### Kuandika sentensi fupi kwa kuzingatia alama za uandishi

Katika somo hili utaandika sentensi fupi. Utazingatia alama nne za uandishi.

**Mfano**

1. Juma, Roza na Hamisi wanacheza mpira.
2. Wanafunzi wameandika vizuri.
3. Laa! ameumia sana.
4. Je, unaweza kuandika mwandiko wa kuunga?


FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 29 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Chunguza alama za uandishi katika sentensi kwenye picha.









Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 30
20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza

Andika alama za uandishi ulizoziona katika sentensi kwenye picha.

1. ..................................................................
2. ..................................................................
3. ..................................................................
4. ..................................................................

## Zoezi la pili

Andika alama za uandishi zilizotumika katika sentensi hizi.

1. Jana timu yetu ya mpira wa miguu ilishinda.
2. Je, tulishinda kwa magoli mangapi?
3. Tulishinda magoli matatu kwa mawili.
4. Loo! Mechi ilikuwa ngumu sana.

## Zoezi la tatu

A. Weka alama za uandishi panapohitajika katika sentensi hizi.

1. Je ni nani aliyeandika ubaoni
2. Loo Mwalimu wetu ameumia mguu
3. Juma Maria Asha na Baraka hawamo darasani
4. Aah Hamisi ni msafi sana
5. Ugali wali na dagaa ni vyakula vitamu
6. Je unapenda michezo yote

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 31 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

B. Andika sentensi tano kisha weka alama za uandishi.

1. ........................................................................
2. ........................................................................
3. ........................................................................
4. ........................................................................
5. ........................................................................

## Somo la pili

### Kuandika habari kwa kuzingatia alama za uandishi

Katika somo hili utaandika habari kwa kufuata mtiririko wa matukio. Utazingatia alama za uandishi

### Zoezi la nne

Andika alama za uandishi zilizotumika katika habari hii.

Jana timu yetu ya mpira wa miguu ilishinda. Usifikiri ilikuwa kazi rahisi, la hasha! Timu ya upinzani ilikuwa imara. Aidha, timu yao ilikuwa makini zaidi kuliko yetu. Timu yetu ilishinda kwa shida. Je, unafikiri tulishinda kwa magoli mangapi? Tulishinda magoli matatu kwa mawili.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 32 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zoezi la tano

Andika habari hii kisha weka alama za uandishi.

Malaria ni ugonjwa hatari unaoenezwa na mbu ili kujikinga na ugonjwa wa malaria ni lazima tulale ndani ya chandarua chandarua bora ni kile kilichowekwa dawa vilivile ni lazima kusafisha mazingira yetu siku zote kwani mbu huzaliana zaidi kwenye madimbwi ya maji machafu.

## Somo la tatu

### Kunakili hadithi na kuweka alama za uandishi

Katika somo hili utanakili hadithi fupi utazingatia alama nne za uandishi.

### Zoezi la sita

Ali ni mwanafunzi katika Shule ya Msingi Mapinduzi anasoma darasa la pili ana miaka nane siku moja Ali alitoroka shuleni kwenda porini kutafuta asali loo aliona mzinga mzuri wenye asali nyingi Ali aliingiza mkono ili achukue asali ghafla Ali alihisi maumivu makali kwenye mkono wake nyuki walimshambulia Ali alilia sana kwa uchungu kutoka siku hiyo Ali hakutoroka tena shuleni pia aliacha tabia ya kuwachokoza nyuki

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 33 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Kuandika habari fupi

Katika sura hii utatunga na kuandika habari fupi. Utatumia picha na chati ya maneno.

## Somo la kwanza

### Kuandika hadithi kwa kutumia picha

Katika somo hili utaandika hadithi yenye kueleweka kwa kutumia picha.

**Soma habari hii kisha fanya zoezi la kwanza.**

### Adelina



FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 34 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Adelina ni msichana wa miaka tisa. Anasoma darasa la pili. Anaishi na bibi yake katika mkoa wa Katavi. Adelina anajituma sana. Kila siku huamka saa kumi na mbili asubuhi. Humsaidia bibi yake kufanya kazi mbalimbali. Baada ya hapo, Adelina hupiga mswaki. Kisha huoga na kuchana nywele. Saa moja kamili Adelina huvaa sare ya shule. Saa moja na robo anakuwa tayari amefika shuleni. Majirani wanamsifu sana Adelina kwa tabia yake nzuri.

### Zoezi la kwanza

Andika hadithi fupi yenye mtiririko mzuri wa matukio.

## Somo la pili

### Kuandika habari fupi

Katika somo hili utaandika habari fupi yenye kueleweka.

Andika habari ifuatayo kisha jibu maswali.

### Tusikate miti ovyo.

Hapo zamani kijiji cha Mbesa kilikuwa maarufu sana. Kilikuwa na misitu yenye miti mikubwa. Mzee Mkwavi aliishi katika kijiji hicho. Wanakijiji walikuwa wanafanya biashara ya mkaa. Waliingia msituni kuchoma mkaa bila utaratibu. Walikata magogo na kuyachoma mkaa. Walitumia panga na shoka kukata magogo.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 35 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Miaka michache baadaye, miti karibu yote ilikuwa imekatwa. Kijiji kilibaki jangwa. Mimea na mito yote ilikauka.

## Zoezi la pili

Jibu maswali haya.

1. Je, kwanini kijiji cha Mbesa kilikuwa maarufu?
2. Mzee Mkwavi alifanya kazi gani?
3. Baada ya miti yote kukatwa kilitokea nini?
4. Unajifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?
5. Nakili aya ya pili kwa mwandiko wa kuunga.

## Zoezi la tatu

Linganisha maneno ya safu mbili ili yalete maana.

| | **Safu A** | **Safu B** |
|---|---|---|
| **1.** | Zamani | Maji yanayoibuka kutoka ardhini |
| **2.** | Gogo | Sehemu kubwa iliyoota miti mingi mikubwa |
| **3.** | Mkaa | Siku nyingi zilizopita |
| **4.** | Msitu | Kipande cha mti mkubwa |
| **5.** | Chemchemi | Kipande cha mti kilichounguzwa |

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 36 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la nne

Chagua neno katika kisanduku kujaza nafasi wazi

mvivu, maneno, karatasi, kucheza, mwandiko, darasa, bidii, hodari, kalamu, Issa.

Siku moja mwalimu wetu alikuwa akitufundisha darasani. Issa alichukua ...................... na ...................... akaanza kuandika. Mwalimu alitufundisha kuandika ...................... kwa mwandiko wa kuunga. Amina ni mmojawapo aliyesoma na ............................. Walisoma ...................... moja. Amina alipenda sana ...................... wa kuunga. Alijifunza kwa ...................... na baadae alikuwa ...................... katika kuandika. Mwalimu alituambia tuwe watulivu tunapofundishwa kuandika.

FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 37 20/08/2021 12:20


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Somo la pili

### Kuandika habari kwa kutumia picha

Katika somo hili utaandika habari fupi kwa kutumia picha.

Mfano wa kuandika habari kwa kutumia picha.



Huyu ni Adamu. Anaishi Chang'ombe mkoani Dodoma. Anatengeneza viti, meza na vitanda. Anapenda kuwa mbunifu katika kazi yake ya useremala. Mwaka jana Adamu alitengeneza madawati mia moja. Alipata zawadi ya kuwa seremala bora wa mwaka.



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 38 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Tazama picha hizi kisha fanya zoezi la tano.**

1.



2.



FOR ONLINE USE ONLY



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 39 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3.



4.



## Zoezi la tano

1. Andika sentensi moja kwa kila picha.
2. Andika habari yenye aya mbili kwa kila picha. Hakikisha unazingatia alama za uandishi.



Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 40 20/08/2021 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la sita

### Habari

Msomee mwenzako habari hii, kisha yeye aiandike. Baadaye na yeye atakusomea na wewe utaiandika.

Maji ni muhimu sana kwa binadamu. Ni sawa na kusema, maji ni uhai. Bila maji hakuna kiumbe hai kinachoweza kuishi. Maji kwa binadamu yana matumizi mbalimbali. Matumizi hayo ni kuoga, kupikia, kufulia na kunywa. Maji ya kunywa lazima yawe safi na salama. Ukinywa maji yasiyo salama unaweza kupata magonjwa. Magonjwa hayo ni kipindupindu na homa ya matumbo. Ni muhimu kuchemsha maji ya kunywa na kuyachuja.

## Zoezi la saba

Jibu maswali haya.

1. Kichwa cha habari uliyosikiliza kinaweza kuwa nini?
2. Taja matumizi ya maji kwa binadamu.
3. Kwa nini ni muhimu kuchemsha maji ya kunywa?

FOR ONLINE USE ONLY




Kuandika std 2_01 March 2018_Kamishna(B5) Final.indd 41 20/08/2021 12:20


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


FOR ONLINE USE ONLY


## Vitabu vingine kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania


### Darasa la Kwanza





















### Darasa la Pili













### Darasa la Tatu















ISBN 978-9976-61-702-3

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*